



Kumb No:TR20220215/01

## TAARIFA KWA WANACHAMA NA UMMA

### TARATIBU ZA UCHAGUZI MKUTANO MKUU TANRIKS 2022

Kwa kuzingatia kuwa Mkutano Mkuu Tanriks 2022 utajumuisha uchaguzi wa viongozi, Kamati Kuu ya Tanriks kuitia mkutano wake Kumb.TR20220213/01, imetoa utaratibu na kanuni zitakazo zingatiwa katika Mkutano Mkuu na uchaguzi utakaofanyika tarehe 26 Machi 2022, Jijini Malmö.

Kamati Kuu inawaomba wanachama wote kuzingatia kanuni na taratibu hizi ili kuhakikisha kuwa Mkutano Mkuu na Uchaguzi, unafanyika kwa haki, amani na usawa kwa wanachama wote.

Kanuni:

1. Mkutano Mkuu na Uchaguzi wa Tanriks 2022 utaendeshwa kwa kuzingatia Katiba ya Tanriks kifungu namba 22 – TARATIBU ZA UENDESHAJI WA MKUTANO MKUU.
2. Kwa kuzingatia kifungu namba 7 cha Katiba ya Tanriks -HAKI, FAIDA NA WAJIBU WA MWANACHAMA. Kifungu kidogo 7.1 na 7.5. Mwanachama anatakiwa awe amelipa Ada zake zote za uanachama toka alipojiunga Tanriks, ili kuweza kuchagua au kuchaguliwa katika Uongozi.
3. Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha wanachama wengi katika uchaguzi, wanachama wanatakiwa kukamilisha kulipa Ada zao tarehe 28 Februari 2022, ili kuweza kujumuishwa katika listi ya wapiga kura kwa uchaguzi wa tarehe 26 Machi 2022.
4. Hakutakuwa na uwezekano kwa mwanachama kuingizwa katika listi ya wapiga kura kwa watakaolipa Ada baada ya tarehe 28 Februari 2022.
5. Wanachama wote watakaolipa Ada baada ya tarehe 15 Februari 2022, wana wajibu wa kutunza risti zao za malipo za kidigital. Na kuwa nazo katika ukumbi wa mkutano kwa kukaguliwa endapo kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo.
6. Ada za vyama wanachama hazitatumika kutoa nafasi kwa mwanachama kuchagua au kuchaguliwa katika Uongozi wa Tanriks. Wanachama wote watatakiwa kulipa Ada zao kibinaksi kwa kuzingatia kifungu namba 7.1 na 7.5 cha katiba ya Tanriks, ili kushiriki katika zoezi la uchaguzi wa viongozi wa Tanriks tarehe 26 Machi 2022.

7. Ulipaji wa Ada ufanyike kwa Swish no. 1230227694 au SEB Bank Akaunti No. 5271176554 au kidigital kupitia link hii: Member Login – TANRIKS. Kwa msaada wa Tehama katika kukamilisha malipo tafadhali piga simu kwa WhatsApp +46724511963
8. Kwa kuzingatia umuhimu wa kufanikisha zoezi la kuingiza wanachama wote waliolipa Ada katika listi ya wapiga kura, wanachama watakoalipa Ada zao kuanzia tarehe 15 Februari 2022 hadi tarehe 28 Februari 2022 wana wajibu wa kumjulisha Mtunza Hazina mara tu watakapo kamilisha malipo yao.  
Kumjulisha Mtunza Hazina unaweza kutuma uthibitisho wa malipo yako kwa barua pepe hazina@tanriks.com au whatsApp +46760558079.
9. Majina ya wanachama watakoopiga kura yatatolewa kwa Umma muda wowote baada ya tarehe 03 Machi 2022 au wiki moja kabla ya tarehe 26 Machi 2022.
10. Majina ya wanaoomba uongozi yatatolewa kwa umma muda wowote baada ya tarehe 16 Februari 2022.
11. Wasimamizi wa uchaguzi watachaguliwa katika Ukumbi wa mkutano kabla ya kuanza zoezi la upigaji kura.
12. Uchaguzi wa Mkaguzi wa Fedha wa ndani, utafanyika katika ukumbi wa mkutano kabla ya uchaguzi wa viongozi.
13. Upigaji kura utafanyika katika ukumbi wa mkutano, watakao ruhusiwa kupiga kura ni wanachama Hai tu, waliokuwepo kwenye listi ya wapiga kura.
14. Uchaguzi wa Tanriks utaendeshwa kwa kuzingatia pia misingi ya kidemokrasi na sheria za usajili wa vyama vyaa kijamii za Sweden.
15. Wanachama na washiriki wengine wote wa Mkutano Mkuu wa Tanriks 2022, wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao na kulipa Ada ya ushiriki SEK 200, kabla ya Tarehe 15 Machi 2022. Kulipa Ada yako tumia Tanriks Swish no. 1230227694 na mjishe Mtunza Hazina kwa WhatsApp no. +46760558079.
16. Mwanachama alieyeomba uongozi ana wajibu wa kutekeleza yafuatayo.
  - a. Kuwepo katika ukumbi wa Mkutano.
  - b. Kujielezea kwa dakika tatu kwa wapiga kura katika ukumbi wa mkutano.
  - c. Kujibu maswali manne kutoka kwa wanachama.

- d. Kuhakikisha kuwa amelipa Ada zake zote za uanachama toka alipojiunga Tanriks kabla ya tarehe 1 Machi 2022.
- e. Kuzingatia taratibu zote za maandalizi ya Mkutano Mkuu 2022.

17. Kwa mawasiliano zaidi tafadhali tumia barua pepe [info@tanriks.com](mailto:info@tanriks.com)

Tanriks inatanguliza shukrani kwa ushirikiano mnaotupatia, na kuwatachia afya njema na ushiriki mzuri katika Mkutano Mkuu 2022. Asanteni sana.

Tanriks inawaleta Watu Wote Pamoja

*Nyegabunaku*

Adolph N. Makaya  
Katibu Mkuu  
Tanriks  
2022-02-15



*Pedersen*

Elizabeth Pedersen  
Mwenyekiti  
Tanriks  
2022-02-15

Nakala: Mhe. Balozi Grace M. Olotu.  
Mlezi Tanriks.  
Ubalozi wa Tanzania  
Stockholm  
Sweden.

3/3